

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

HALMASHAURI YA WILAYA YA SAME

SHULE YA SEKONDARI CHALAO



SHULE YA SEKONDARI CHALAO,

S.L.P 333,

SAME.

Mob:0656649563

15/12/2020.

KUMB.NA.CHSS.....

JINA LA MWANAFUNZI.....

S.L.P.....

YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI CHALAO 2021

1.0 UTANGULIZI:

Nafurahi kukujulisha kuwa umechaguliwa kujiunga kidato cha **KWANZA** katika Shule ya Sekondari Chalao. Tunakupongeza kwa mafanikio hayo.

Shule itafunguliwa rasmi tarehe **11/01/2021** unatakiwa kuwepo shuleni siku hiyo. Kutofika shule kwa wakati uliopangwa kunaweza kukupotezea nafasi yako ya masomo. Shule iko wilaya ya Same, Mkoa wa Kilimanjaro.

2.0: MAELEKEZO MAALUM YA KUZINGATIA

2.1: SARE ZA SHULE

2.1(A): WAVULANA: i) Mashati mawili meupe mikono mifupi aina ya tomato.

ii) Suruali mbili, moja rangi **nyeusi** na ya pili rangi ya **kijani**

iii) Tai mbili, moja rangi **nyeusi** na ya pili rangi ya **kijani**

iv) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba visiwe na visigino virefu.

v) Soksi nyeupe pea mbili.

vi) Mkanda mweusi wa kuvalia suruali wa ngozi na wenye bakoli ya kawaida.

vii) Suruali zishonwe pana, inch 15 upana na ziwe na marinda mawili, zenye pindo la "turn up".

NB: Tafadhali zingatia rangi ya vitambaa vilivyoambatanishwa na fomu hii, suruali inayobana, isiyovalika kiunoni na isiyofuata maelekeo hapo juu haitakubaliwa.

2.1(B): WASICHANA: i) Mashati mawili meupe mikono mifupi aina ya tomato.

ii) Sketi mbili, moja rangi **nyeusi** na ya pili rangi ya **kijani**

iii) Tai mbili, moja rangi **nyeusi** na ya pili rangi ya **kijani**

iv) Viatu vyeusi vya kufunga na kamba visiwe na visigino virefu.

v) Soksi nyeupe pea mbili.

vi) Sketi ndefu mshono marinda,mbele marinda sita na nyuma sita jumla 12.

vii) Belti inch mbili ziwe ndefu za kutosha,pana na ziwe za kuvalia kiunoni.

NB: Tafadhali zingatia rangi ya vitambaa vilivyoambatanishwa na fomu hii,sketi inayobana,isiyovalika kiunoni na isiyofuata maelekeo hapo juu haitakubaliwa.Pia aina ya kitambaa ni ESTEM No.1.

2.1(C): SARE NYINGINE:

- Sare ya michezo ni T.shirt ya rangi ya **light bluu**,bukta ya rangi **light bluu** na raba za rangi yoyote kwa wavulana.
- Sare ya michezo ni T.shirt ya rangi ya **light bluu** na tracksuit rangi **light bluu** na raba za rangi yoyote kwa wasichana.
- Sweta ni za rangi **nyeusi** mshono wa V mbele.Hijabu kwa wasichana iwe nyeupe aina ya Tetron,kubwa ya kufunika kifua.

2.2: VIFAA VYA KITAALUMA: Mwanafunzi aje na Daftari "counter book quire two" tisa,kalamu za kutosha,mkebe na "Dictionary English to English by Oxford,Graph pad 01 na begi jeusi la mgongoni la kubebea madaftari.

2.3: CHAKULA CHA MCHANA NA UJI:Kila mwanafunzi atachangia mahindi kilo 40,maharage kilo 20 kwa mwaka,pia shilingi 20,000/= kwa ajili ya kulipa mpishi na kununua mafuta,sukari na huduma ya kusaga,pia taaluma 10,000/=kwa ajili ya walimu wanaolipwa na wazazi.

2.4: VIFAA VYA USAFI:

i) Wavulana waletе slesha moja na ufagio wa ukindu.

ii) Wasichana waletе mopa na ufagio wa ukindu..

3.0: VIAMBATA:Kila mwanafunzi anatakiwa kusoma vyema maelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yote yaliyomo kwenye viambata vifuatavyo **A-E:**

- A. Sheria,kanuni na taratibu za Shule,(atazikuta shuleni)
- B. Fomu ya kupimwa Afya toka kwa mganga hospitali ya serikali(medical examination form)
- C. Ahadi/kiapo cha Mwanafunzi kukubaliana na sheria na maelekezo ya shule,Mzazi atathibitisha(ataikuta shuleni)
- D. Fomu ya Utambulisho wa Mwanafunzi(ataikuta shuleni)
- E. Mzazi atakapo mleta mtoto shuleni aje na passport size moja ya hivi karibuni.

Tarehe ya mwisho kuripoti Shuleni ni tarehe **18/01/2021**.

KARIBU SANA CHALAO SEKONDARI

STEVEN JUSTIN MSUYA

MKUU WA SHULE.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI CHALAO



S.L.P 333,

SAME-

MOB.NA : 0656649563

KILIMANJARO.

KIAMBATA B: MEDICAL CERTIFICATE FORM

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION OF.....FORM **ONE**

Please examine the above named as to his fitness for admission to school as a student.

Name of requesting officer: STEVEN J.MSUYA Date: 15/12/2020

To be completed by a Government Medical Officer.

Student's Full Name:

Blood count (red and white).....

Stool examination.....

Urinalysis.....

Syphilis Test.....

T.B Test.....

Eye Test.....

Ears.....

Chest.....

Spleen.....

Abdomen.....

Blood group.....

ADDITION INFORMATION e.g Physical defects or impairments, infections, chronic or family diseases etc.....
.....

I have examined the above named and I consider that he/she is physically fit/unfit to pursue as stated above.

Name and signature of Certifying Officer,Name.....

Signature.....

Station..... Designation.....

Date..... STAMP.....

1.0 SHERIA NA KANUNI ZA SHULE HII

Shule inaendeshwa kwa mujibu wa sheria ya elimu Na. 25 ya mwaka 1978 na kama ilivyorekebishwa kwa sheria Na.10 ya mwaka 1995. Aidha inazingatia miongozo yote inayotolewa na wizara ya elimu na mafunzo ya ufundi, yenye dhamana ya elimu nchini na ofisi ya Raisi- TAMISEMI yenye jukumu la usimamizi na uendeshaji Elimu.

unatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo:

- a) Heshima kwa viongozi , wazazi,wafanyakazi wote,wanafunzi wengine na jamii kwa ujumla ni jambo la lazima.
- b) Mahudhurio mazuri katika kila shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima.
- c) Kushiriki kwa makini kufanya maandalio ya jioni (preparation)
- d) Kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopewa.
- e) Kufahamu mipaka ya shule na kuzingatia kikamilifu maelezo juu ya kuwepo ndani na nje ya mipaka hiyo wakati wote wa uanafunzi wako katika shule hii.
- f) Kutunza usafi wa mwili , mavazi na mazingira ya shule.
- g) Kuvaa sare ya shule wakati wote unapotakiwa
- h) Kuzingatia ratiba ya shule wakati wote na
- i) Kutunza mali za umma.

3.1. MAKOSA YAFUATAYO YANAWENZA KUSABABISHA KUFUKUZWA AU KUSIMAMISHWA SHULE

- a) Wizi
- b) Uasherati na Ushoga
- c) Ubakaji
- d) Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kuberi na kadhalika.
- e) Kupigana au kupiga.
- f) Kuharibu kwa makusudi mali ya umma.
- g) Kudharau bendera ya taifa.
- h) Kuwa Mjamzito/Kupata Mimba
- i) Kuoja Au Kuolewa.
- j) Kutoa Mimba.
- k) Kusababisha Mimba/Ujauzito ndani na Nje Ya Shule
- l) Kugoma, Kuchochea na Kuongoza Au Kushiriki Kuvuruga Amani na Usalama wa shule au Watu.
- m) Kukataa adhabu kwa makusudi
- n) Kuwa na Simu ya Mkononi.

2.0 MAMBO MENGINE MUHIMU YANAYOPASWA KUKAMILISHWA SHULENI NA MWANAFUNZI ANAPORIPOTI

- A. Medical examination form ambayo itajazwa na mganga mkuu wa Hospitali ya serikali. fomu itakabidhiwa kwa mkuu wa shule mara utakaporipoti shuleni.(fomu imeambatanishwa)
- B. Fomu ya maelezo binafsi kuhusu historia ya mwanafunzi na mkataba wa kutoshiriki katika migomo, fujo na makosa ya jinai. (fomu imeambatanishwa)
- C. Fomu ya mzazi kukiri kukubaliana na sheria, kanuni na maelekezo mengine yatakayotolewa na shule.(fomu imeambatanishwa)
- D. Ahadi/kiapo cha Mwanafunzi kukubaliana na sheria na maelekezo ya shule,Mzazi atathibitisha(atafikuta shuleni)

3.0 Tafadhali soma kwa umakini maelekezo/maagizo haya na kuyatekeleza kikamilifu.

KARIBUNI SANA KATIKA SHULE HII

.....
STEVEN J. MSUYA

MKUU WA SHULE

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA WAZIRI MKUU TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

SHULE YA SEKONDARI CHALAO P.O.BOX 333

Phone : 0656649563

AHADI/ KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi Ambaye nimechaguliwa kujiunga na SHULE YA SEKONDARI CHALAO KIDATO CHA KWANZA mwaka 2021 ninaipokea na kukubali nafasi niliyo pewa kwa malengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo ya Taifa na Shule ya Sekondari ya Chalao.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.

Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapo shuleni:

- i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yangu.
 - ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazo kuwa zikitolewa mara kwa mara.
 - iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni.
 - iv. Ikiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudi nyumbani kumwita mzazi/ mlezi wangu (Jina la mzazi) kwa ajili ya hatua zaidi.
- Saini ya mwanafunzi tarehe

SEHEMU YA MZAZI/MLEZI

Mimi ninakubali mtoto wangu Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari Chalao mwaka 2021. Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa taifa. Anuani yangu ya kudumu ni

Simu Iwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi nilazima nitajulisha shule kwa maandishi

Saini ya Mazazi/MleziTarehe

WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI
SHULE YA SEKONDARI CHALAO S.L.P 333, SAME
TAARIFA BINAFSI YA MWANAFUNZI

Jina la mwanafunzi (Majina matatu)

Shule ya msingi anapotokatarehe ya kuzaliwa..... mwezi

Mwaka tarehe ya kuripoti shuleni

Makazi :- kijijikitongoji

TAARIFA YA WAZAZI

1. BABA

a) Jina la baba (Yu hai/ Amefariki)

b) Anwani yake

- c) Kazi yake
- d) Dini yake: (Mkristo/ Mwislamu)Dhehebu
- e) Makazi : KijijiKitongoji


2. MAMA

- a. Jina la mama (Yu hai/ Amefariki)
- b. Anwani yake
- c. Kazi yake
- d. Dini yake: (Mkristo/ Mwislamu)Dhehebu
- e. Makazi : KijijiKitongoji

3. MLEZI

- a) Unaye mlezi ? (Mlezi ni mtu ambaye si mzazi lakini anakulea, kukutunza na kukupatia mahitaji yote ya nyumbani na shule.....
- b) Jina la mlezi
- c) Anwani ya mlezi
- d) Dini yake: (Mkristo / Mwislamu) Dhehebu
- e) Makazi : KijijiKitongoji
- f) Uhusiano wa mlezi na mwanafunzi

FOMU YA MZAZI KUKIRI KUKUBALIANA NA TARATIBU MBALIMBALI ZA SHULE



Mimi(Jina la mzazi /mlezi halisi) ambaye
 picha yangu imebandikwa hapo juu, ni mzazi /mlezi halisi wa mwanafunzi
 Kidato chamwaka

Nakiri kukubaliana na sheria , kanuni, kulipa michango mengine na maelekezo mengine yote yatakayotolewa na shule kwa ajili ya maendeleo ya mwanangu.

Natambua kuwa kushindwa kukamilisha taratibu hizi kwa wakati kutachochea kurudisha maendeleo ya mwanangu nyuma.

Jina sahihi